

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 2 Novemba, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA  
MASHARIKI**

*(Hapa Kwaya ya Bunge iliimba Wimbo wa Taifa na Wimbo  
wa Jumuiya ya Afrika Mashariki)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaweza tukakaa. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa:-

1. Mhe. Dkt. Elieza Mbuki Feleshi;
2. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani; na
3. Mhe. Mohamed Said Issa.

**SPIKA:** Katibu.

## **NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

### **TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba aliyejikuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji Mheshimiwa William Tate Olenasha alifariki tarehe 27 Septemba, 2021 Jijini Dodoma. Waheshimiwa Wabunge hayati William Tate Olenasha aliagwa rasmi katika Viwanja vya Bunge Jijini Dodoma tarehe 30 Septemba, 2021 na kuzikwa jimboni kwake tarehe 02 Oktoba, 2021. Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa leo ni siku ya kwanza Bunge linakutana tangu msiba huo mzito utokee kwa heshima naomba tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka na kumuombea Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika  
moja ili kumkumbuka na kumuombea  
Marehemu Mheshimiwa William Tate Ole Nasha)*

**SPIKA:** Bwana ametoa, Bwana ametwaa, jina Lake lihimidiwe, amina. Ahsanteni.

Taarifa ya pili, naomba niwataarifuni Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Mkutano wa Nne wa Bunge, Bunge lilipitisha miswada mitano ya Sheria ifuatayo: -

(i) Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.3 wa mwaka 2021; *[The written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 3) Bill, 2021]*.

(ii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.4 wa mwaka 2021 *[The written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 4) Bill, 2021]*.

(iii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Mwaka 2021 *[The Accountants and Auditors Registration (Amendment) Bill, 2021]*.

(iv) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 [*The Fire and Rescue Force (Amendment) Bill, 2021*].

(v) Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.5 wa mwaka 2021 [*The written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 5) Bill, 2021*].

Kwa taarifa hii sasa, napenda kuwataarifuni Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo mitano imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Muungano wa Tanzania na kuwa Sheria za Nchi. (*Makofi*)

Sheria hizo za Nchi zinaitwa:-

(i) Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 3 ya Na. 5, ya mwaka 2021; [*The written Laws Miscellaneous Amendment No.3 Act No. 5 of 2021*].

(ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.4 ya 6 ya mwaka 2021; (*The written Laws Miscellaneous Amendment No. 4, Act No.6 of 2021*).

(iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Na. 7 ya mwaka 2021; (*The Accountants and Auditors Registration Amendment Act No. 7 of 2021*).

(iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Na. 8 ya Mwaka 2021; (*The Fire and Rescue Force Amendment Act No. 8 of 2021*).

(v) Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 ya 9 ya mwaka 2021; (*The written Laws Miscellaneous Ammendments No. 5 Act No. 9 of 2021*).

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

## **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Sasa ni kipindi cha maswali; na aliyebahatika kutuongoza kwa swali la kwanza siku ya leo ni kuelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, naye si mwingine bali ni Mheshimiwa Issa J. Mtemvu, Mbunge wa Kibamba. Mheshimiwa Issa Uliza swali lako.

Na.1

### **Ujenzi wa Barabara ya Mbezi Shule – Mpiji Magohe kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Mbezi Shule – Mpiji Magohe – Bunju kupitia Mabwe Pande na Kibamba Njia Panda – Mpiji Magohe kama zilivyoainishwa kwenye llani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.

**SPIKA:** Majibu ya Swali hilo, Mheshimiwa *Engineer Godfrey K. Msongwe*, tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa J. Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbezi Shule – Mpiji Magohe – Bunju kupitia Mabwe Pande ni barabara inayotambulika kwa jina la Mbezi Victoria – Mpiji Magohe hadi Bunju yenye urefu wa kilometra 25; na barabara ya Kibamba Njia Panda – Mpiji Magohe inatambulika kwa jina la Kibamba Shule hadi Mpiji Magohe ambayo ina urefu wa kilometra 8.7.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni sehemu ya barabara ya Mzunguko wa Nje wa jiji la Dar es Salaam (*Outer Ring Roads*) inayoanzia Bunju – Mpiji Magohe – Kibamba –

Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma mpaka Kigamboni ambayo ina urefu wa kilometra 61.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika mpango wa kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 jumla ya Shilingi milioni 600 zimetengwa kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya mzunguko wa nje inayoanzia Bunju – Mpiji Magohe – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma mpaka Kigamboni na mzunguko wa ndani inayoanzia – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara hadi Kigamboni. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wakufanya kazi hiyo zipo katika hatua za mwisho za uchambuzi wa zabuni. Mara baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa nimkuona, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa majibu mazuri yametolewa na Serikali, kwa umuhimu barabara hizi pamoja na kuondoa msongamano sehemu ya pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam lakini pia zinasaidia kufungua uchumi wa wananchi wa pembezoni. Aidha, barabara hizi zilipata baraka za Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na kuzitamani zijengwe kwa haraka na udharura. (*Makofi*)

Je, Serikali sasa haioni inayo kila sababu kukamilisha barabara hizi katika mwaka wa fedha 2022/2023? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kilomita zilizotajwa 33.7 ina sehemu ya kilometra 1 ya barabara ya njiapanda ya shule na wanahitaji fidia. Je, Serikali imejipanga vipi kulipa fidia wananchi hawa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, Mheshimiwa Msongwe.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu Mbunge wa Kibamba kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika ni kweli kwamba Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais aliahidi kwamba, barabara za Jimbo la Kibamba angetamani zijengwe zote kwa kiwango cha lami. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wa Kitaifa, zote tunazichukulia kwa umuhimu mkubwa sana na ndio maana hata akienda kwenye kitabu chetu cha bajeti, tumetenga tayari fedha, kwa ajili ya kuanza upembuzi kwa sababu, barabara zote zilizotajwa katika Jimbo lake ni za vumbi. Kwa hiyo, lazima hatuwezi tukaruka hatua ni lazima tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na uhakika kwamba tunatambua pia tutafungua uchumi wa Jimbo lakini pia kurahisisha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii la pili nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kawaida barabara zote zinapojengwa tutahakikisha kwamba hiyo fidia aliyoitaja, tunailipa kabla ya ujenzi na kama kuna changamoto zaidi ya hii ambayo tunafahamu ya kuilipa kwa kawaida, basi nimuombe Mheshimiwa Mbunge tuweze kuonana naye kwa ajili ya kupata maelezo zaidi. Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonist swalii la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Barabara ya Murongo kuja Kibale kuja Bugara halafu mpaka Mgakorongo ni barabara ya hadhi ya Mkoa. Ikiunganisha Uganda na Tanzania na mchakato wake umechukua muda mrefu. Nataka kujua ni lini hiyo barabara itaanza kujengwa kwa sababu, imekuwepo mchakato wake muda mrefu. Nataka kujua Serikali imejipangaje? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhalii.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI – (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara iliyotajwa ni barabara kuu na ni barabara ambayo ni kweli inaunganisha Tanzania na Uganda katika lile eneo linaloitwa Murongo. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara ile nimeitembelea na barabara hiyo kwa mwaka huu, imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza kwa kiwango cha lami ujenzi huo. Kwa hiyo, nimuhakikishie kwamba ipo kwenye mchakato na barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Shamsia Mtamba uliza swali lako.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kutokana na umuhimu wa barabara inayotoka Mtware mjini kuelekea Msimbati, ambako kuna visima na mitambo ya gesi. Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Godfrey Msongwe*, tafadhalii.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja ni barabara muhimu kwa sababu inaenda kwenye maeneo ya kimkakati. Naomba nimuhakikishie kwamba kadri fedha itakavyopatikana katika bajeti zinapokuja, barabara hii tutajenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tunaifahamu ni

barabara muhimu kutegemea na upatikanaji wa fedha na hasa kwa bajeti ambayo tutaanza kuitengeneza mwezi wa tatu mwakani. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Tunaendelea bado tuko Wizara hii hii Waheshimiwa Wabunge. Sasa ni barabara ya Nyamisati swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Ally Mpembenwe. Mheshimiwa Mpembenwe tafadhalii.

Kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa uliza swali hilo.

Na. 2

**Ujenzi wa Barabara ya Nyamisati – Bungu**

**MHE. SUBIRA K. MGALU K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuiliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa barabara ya Nyamisati hadi Bungu katika Jimbo la Kibiti?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri bado tuko na wewe Mheshimiwa Godfrey.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bungu – Nyamisati yenye urefu wa kilometra 40.2 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) iliyopo katika Wilaya ya Kibiti, Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Serikali kuititia Wakala wa Barabara Tanzania, imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa

barabara hii. Taratibu za kumpata mshauri elekezi wa kufanya kazi hiyo, ziko katika hatua za mwisho za kusaini mkataba. Baada ya usanifu kukamilika na gharama kujulikana Serikali itatafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na maandalizi ya kujengwa barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania, inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii. Ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka na katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022 jumla ya Shilingi milioni 732.67 zimetengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge viti maalum Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Subira Mgusu nimekuona.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa majibu mazuri yenye kutia matumaini ya wakazi wa Jimbo la Kibiti. Hususani walio jirani na barabara ya Bungu Nyamisati kwa kuwa Serikali imetenga fedha, ya kuanza upembuzi yakinifu na hizi milioni 700 kwa ajili ya matengenezo ili ipitike muda wote.

Mheshimiwa Spika naomba sasa niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika hilo Jimbo la Kibiti kuna barabara muhimu ya Kibiti Dimani Mloka ambapo pia, magari yanayoelekea kwenye mradi muhimu wa kimkakati wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere wanaitumia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza upembuzi yakinifu kwa kuwa barabara hii pia ipo kwenye ilani ya uchaguzi ya mwaka 2025, kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami? Ili kuwezesha ipitike muda wote kuelekea kwenye Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.  
GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Subira Mgali Mbunge wa Viti Maalum Pwani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara aliyoitaja ni kati ya barabara ambazo zinapika kwenye mradi wetu wa kimkakati na imeainishwa kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi kama alivyosema ambayo ni ya 2020 – 2025. Naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara zote ambazo zimeainishwa katika ilani haziwezi zote zikatekelezwa kwa mwaka mmoja. Lakini nimuhakikishie kwamba zipo kwenye mpango na zitafanyiwa upembuzi yakini na usanifu wa kina, kama ilivyoainishwa kwenye ilani katika kipindi hiki cha miaka mitano. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumalizie kwa sababu ya muda, swalii la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusii.

Na. 3

**Ujenzi wa Barabara ya Igowole Km. 54**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Igowole – Nyigo kilomita 54 ambayo imetajwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA  
M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara ya Mkoa ya Igowole - Kasanga - Nyigo yenye urefu wa kilometa 54.51, inayosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Igowole – Kasanga – Nyigo yenye urefu wa kilomita 54.51 kwa Wananchi wa Wilaya ya Mafinga. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanya upembizi yakinifu na usanifu wa kina na hatimaye kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na juhudzi za kutafuta fedha ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia *TANROADS* inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii, ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi milioni 66 kimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nancy nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, katika ukanda huu kuna barabara tatu ambazo ni Gohole, Nyigu, Mtwango, Nyololo na Mafinga Mgololo.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba barabara hizo zitapitika katika kipindi hiki cha mvua ambazo zinaanza? Kwa sababu hazipitiki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Waitara tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nancy Nyaliusi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo hili Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ameshaji-*commit*. Tulikubaliana kwamba mwaka wa fedha unaofuata 2022/2023 tutaanza kujenga eneo hili kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili naomba nitumie nafasi hii kutoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Iringa, atembelee maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Afanye tathmini na kama kuna shida basi matengenezo yafanyike, wananchi wapate huduma ya usafiri wa miundombinu wakati wote wa mvua. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante tuendelee Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Nora Waziri Mzeru uliza swali lako Mheshimiwa Nora.

Na. 4

#### **Kuwasaidia wafugaji wa Mkoa wa Morogoro**

**MHE. NORA W. MZERU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wafugaji wa Mkoa wa Morogoro kufanya ufugaji wa kisasa na wenye tija kwa kuwa Mkoa huu una wafugaji wengi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri Mifugo na Uvubi, tafadhalii.

#### **NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nora Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali, ili kufanya ufugaji katika Mkoa wa Morogoro kuwa wenye tija na wa kisasa. Juhudi hizo ni pamoja na uboreshaji wa mbari za mifugo kwa kuhimilisha ngómbe, kuwezesha upatikanaji wa kuku wazazi walioboreshwa, mafunzo rejea juu ya teknolojia za ufugaji bora kwa wafugaji na maafisa ugani. Vipindi vya elimu kwa umma vya redio, televisheni, maonyesho mbalimbali yakiwemo ya sabasaba na nanenane.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhud hizi, hadi mwaka 2020 mifugo iliyoboreshwa katika Mkoa wa Morogoro imefikia ng'ombe 28,582 sawa na asilimia 3 ya ng'ombe wote na mbuzi 19,899 sawa na asilimia 11 ya mbuzi wote na kuku millioni 2.5 sawa na asilimia 69 ya kuku wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na wadau na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inatarajia kuhimilisha ng'ombe 32,606 Mkoani Morogoro, kwa kutumia mbegu bora za mifugo za ruzuku kutoka katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC Arusha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nora ameridhika.

**MHE. NORA W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na migogoro ya muda mrefu, baina ya wafugaji na wakulima nchini hususani Mkoa wangu wa Morogoro. Je, Serikali itawasaidiaje wafugaji maeneo ya malisho ili kuepusha migogoro na wakulima? Ahsante. (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nora Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji katika Mkoa wa Morogoro, tunayo *Ranch* yetu ya

Taifa ya Mkata. Tumekwisha kuanza utaratibu wa kuwagawia wafugaji wenyeji wa Mkoa wa Morogoro. Hadi sasa tumeshatoa vitalu saba, kwa ajili ya wafugaji katika eneo hili na utaratibu huu unaendelea. Pia, Wizara inayo mkakati wa maeneo yake ambayo tumekubaliana kwamba, yako chini ya kiwango cha matumizi ikiwemo baadhi ya *Ranch LM News* na *Holding Grounds*. Hizi zote tunazitazama na kuhakikisha kwamba tutazipima na kugawa vitalu baadhi kwa wafugaji walioko maeneo mbalimbali nchini. Ili kuweza kuwasaidia kuondokana na hamahama na kwenda kugombana na wafugaji na wakulima. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Maji swali linaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge wa Mkinga. Mheshimiwa Kitandula uliza swali lako. Endelea kwa niaba.

Na. 5

**Kuvipatia maji Vijiji vya Kwangena, Bantu na Machimboni Wilaya ya Mkinga**

**MHE. JOHN M. SALLU K.n.y. MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuvipatia maji kutoka mradi wa Mapatano Vijiji vya Kwangena, Bantu na Machimboni Wilayani Mkinga?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Winfred Mahundi*, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula Mbunge wa Jimbo la Mkinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha maeneo yote ya vijiji ni huduma ya upatikanaji wa maji inaboreshw. Ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022

kazi ya upanuzi wa skimu ya maji ya Mapatano inafanyika. Ili kufikisha maji katika vijiji vya Kwangena, Bantu na Machimboni ambavyo mahitaji ya maji ni lita 251,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika upanuzi huo kazi zitakazofanyika ni kulaza mabomba Kilomita 29 na kujenga matenki mawili (2) ya kuhifadhi maji lita 45,000 na lita 135,000. Kazi hii inatarajiwu kukamilika mwezi Agosti, 2022 na utanufaisha wananchi takriban 11,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Sallu ameridhika. Waheshimiwa mnapaswa kuwa mnasimama *immediately* vinginevyo namuita mtu mwngine.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini naomba Serikali ituhakikishie kwamba, katika kipindi hicho cha miezi tisa kweli huu mradi unaweza kumalizika maana tuna shida kubwa sana ya maji pale. Ahsante sana.

**SPIKA:** Kifupi sana uthibitisho tu kwamba mradi utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula kwa kuwasilishwa na Mheshimiwa John Sallu kwamba, Serikali tumejipanga ndani ya miezi tisa mradi utakamilika na tunaendelea kuongeza nguvu kuhakikisha ikiwezekana kabla ya miezi (9) kufika iwe imekamilika.

**SPIKA:** Nishati. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare.

Na. 6

**Vijiji vya Manyoni kuondolewa kwenye watumiaji wadogo wa Umeme**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

(a) Je, kwa nini *TANESCO* imewaondoa watumiaji wadogo wa umeme chini ya *unit 75* katika Vijiji vya Itigi, Majengo, Ziginali, Tambukareli, Songambele na Mlowa kuwa Mitaa badala ya Vijiji?

(b) Je, ni lini wanavijiji hao watarudishwa katika matumizi ya watumiaji wadogo kwa kuwa hivi ni Vijiji na si Mitaa?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati. Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, tafadhali.

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Agizo la kurekebisha bei la *EWURA* Na. 2016-010 la Mwaka 2016, kuitia masharti Namba (h) na (i) inaelekeza *TANESCO*, kuwaunganisha wateja wapya wa majumbani walio maeneo ya vijiji katika kundi la D1 yaani *Domestic 1*. Kuitia mfumo wa njia moja ya umeme na wateja walio katika kundi la D1 watahamishiwa kwenda T1 ambayo ni *Tariff 1*. Endapo manunuzi yao katika kipindi cha miezi mitatu mfululizo yatazidi wastani wa *unit 75* kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, wateja wa Itigi walihamishiwa kwenda kundi la T1 kwa kuwa wapo Itigi mjini. Kwa sasa, *TANESCO* inaendelea kuchambua hali ya ununuzi wa umeme kwa wateja hawa. Kwa lengo la kubaini walokidhi vigezo vya kuwa kwenye kundi la D1 kwa mujibu wa Agizo la *EWURA*. Zoezi hili linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 30 Novemba, 2021. Baada ya zoezi hili kukamilika wanaostahili kuwa kwenye kundi la *Tariff D1* watapelekwa kwenye kundi hili Disemba, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Massare nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, lakini yapo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Singida eneo ambalo linaathirika sana na ukatikaji wa umeme ni eneo la Itigi, lakini na Manyoni wao wanaita *feeder* ya Manyoni na kila Jumamosi au Jumapili ya wiki lazima umeme ukatike. Sasa je, ni lini zoezi hili litakoma kukatwa katwa umeme katika Halmashauri ya Itigi?

Mheshimiwa Spika lakini pili tunachangamoto ambayo imetokea sasa wakati wenzetu wanaendelea na wakandarasi wa *REA* nchi nzima katika wilaya ya Manyoni hakuna mkandarasi. je, ni nini tatizo na ni lini mkandarasi wa *REA* /// atapatikana katika Halmashauri za Manyoni na Itigi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Byabato. Kukatika umeme siyo amesema kwamba ni lini umeme hautakatika; amesema lini kukatikakatika umeme kutakoma? Naomba majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Massare kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na swali la pili la Mkandarasi wa *REA*. Ni kweli kwamba Serikali ilitangaza kazi za kutengeneza umeme wa vijijini na maeneo mengi yakawa yamepata wakandarasi, lakini maeneo Matano yalibaki bila kupata wakandarasi ikiwemo Singida kwa maeneo ya Itigi na Manyoni ni mojawapo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwenye Bunge Iako Tukufu kwamba Ijumaa ya wiki iliyopita, Mkandarasi anayeitwa TungTang amesaini mkataba wa kupeleka umeme katika Wilaya zetu za Itigi na Manyoni na

tumemwambia aripoti kazini Jumatatu ijayo wakati sisi ofisini Serikali ikiwa inaendelea kukamilisha utaratibu wa malipo ya awali.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kusema kwamba, lot ya Singida iko pamoja na lot ya Shinyanga, Tanga na Arusha. Wakandarasi wote hawa tunatarajia waanze kuripoti katika maeneo yao ya kazi kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la kukatikakatika kwa umeme, nianze kwa kusema kwamba tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo inaonekana wazi kabisa kwamba kuna mabadiliko makubwa ambayo yamefanyika katika Wizara ya Nishati, lakini katika Shirika letu la TANESCO na tunatarajia kabisa kwamba katika kipindi kifupi kijacho wenzetu ambao wamepewa dhamana sasa *TANESCO* wataenda kukidhi yale mahitaji ambayo Watanzania wanayatarajia.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, bajeti ya TANESCO sasa imewekewa mechanism ya kuhakikisha inaongezeka kwa kuziba ile mianya iliyokuwa ikiachia mapato yavuje ili kuweza kupata nguvu zaidi sasa ya kuimarisha maeneo hayo ya kukatika kwa umeme. Kukatika kwa umeme kunasababishwa na sababu nyingi nyingi, lakini zile ambazo ziko ndani ya uwezo wetu tunahakikisha kwamba tunazifanyia kazi ili tatizo hilo liveze kwisha, siyo kwa Itigi na Manyoni peke yake, lakini kwa nchi nzima. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Nimekuona Mbunge wa Ifakara.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pia Halmashauri ya Mji wa Ifakara Jimbo la Kilombero imekuwa ikikosa umeme kila Jumanne na Alhamis; na tunamradi mkubwa sana wa Serikali wa zaidi ya shilingi bilioni 20 wa kituo cha kukuzia umeme. Ujenzi huo wa mradi unasuasua kwa muda mrefu sana:-

Je, Naibu Waziri atakuwa tayari kutembelea pale kutazama changamoto za kusuasua za mradi ule?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako nipo tayari kwenda kuangalia changamoto hizo, lakini ni seme kwamba kama anasema ni Jumanne na Alhamis, basi nitafanya mawasiliano na wenzangu tufahamu shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, ni wahakikishie Watanzania kwamba hatuna mgao kwa nchi yetu ya Tanzania kwa sasa. Tunao umeme ambao unatosheleza mahitaji tuliyokuwa nayo kwa kile kiasi tunachowenza kupeleka, lakini tutaenda kuangalia tatizo ni nini ili tuweze kulitatuwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali King nilikuona.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kuwa ni swali la msingi liliulizia bei ya umeme, nami niulize ni lini *TANESCO* itatausha bei ya umeme inayouza *ZECO*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali muhimu hilo. Majibu kwa umakini mkubwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ali King kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* kwa maana ya Shirika la Umeme Tanzania imekuwa na mkataba na Shirika la *ZECO* kwa maana ya Shirika la Umeme la Zanzibar kwenye kuuziana umeme. Tumekuwa na bei ambazo zinatofautiana; na tumekuwa tuna majadiliano kwa muda mrefu katika eneo

hili na jambo hili likapelekwa mpaka kwenye kamati zetu zinazoshughulikia maswali ya na Muungano.

Mheshimiwa Spika, *issue* kubwa ilikiwa ni habari ya bei. *TANESCO* walikuwa wanaona wakiiza umeme kwa shilingi 130/= ambayo wenzetu wa *ZECO* wanaihitaji hawataweza kwa sababu itakuwa ni hasara. *ZECO* wanasema sisi tukiwauzia kwa shilingi 156/= ambayo tunaona ni ghamama za chini za kuzalisha, hatutaweza kufanikiwa kwa sababu *ZECO* wanasema hiyo kwao ni ghamama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kumekuwa na mazungumzo yanayoendelea na suala hilo limepelekwa katika Kamati ile inayoshughulikia masuala ya Muungano na tunasubiria maelekezo ya Serikali ili kuona namna gani tunaweza kusaidia mashirika haya mawili yaweze kuendelea kushirikiana na kukamilisha upelekaji wa umeme kwa ghamama nafuu kwa wenzetu wa Zanzibar. (*Makofii*)

**SPIKA:** Bado tupo Wizara hii hii Waheshimiwa Wabunge ya Nishati swali linaulizwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

Na. 7

#### **Ukosefu wa Umeme wa Gridi ya Taifa Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Umeme wa Grid ya Taifa katika Mkoa wa Katavi?

**SPIKA:** Majibu ya swali ilo bado tupo kwako, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati. Tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa Gridi ya Taifa wa msongo wa kilovolti 132 yenye urefu wa kilometra 381 kutoka Tabora hadi Katavi na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vya msongo wa kilovolti 132/ 33kV Ipole (Sikonge), Inyonga (Mlele) na Mpanda (Mpanda Mjini).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majengo ya kudhibiti mfumo wa umeme (*Control Building*) ya Ipole, Inyonga na Mpanda yamekamilika. Upimaji wa mkuza (*wayleave*) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (*Transmission Line*) kutoka Tabora hadi Katavi umekamilika. Zoezi la uthamini wa mali za wananchi katika maeneo yanayopitiwa na mradi limekamilika kwa Wilaya za Mlele na Mpanda Mjini na zoezi hilo linaendelea kwa Wilaya za Tabora, Uyui, na Sikonge na litakamilika mwishoni mwa mwezi wa Novemba, 2021. Mradi unatarajiwaa kukamilika ifikapo Agosti, 2023.

Mheshimiwa Spika, gherama ya mradi ni shilingi bilioni 64.9 na fedha hizi zote ni fedha za ndani na ujenzi unafanywa na Wataalamu wa Shirika la *TANESCO*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska, swali la nyongeza, tafadhalii.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kunipa nafasi kwa kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu umeme ninayo maswali mawili ya nyongeza kwa Mkao wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza wananchi wa Mkao wa Katavi wanahitaji umeme wa gridi kwa haraka ili waweze kujenga viwanda, lakini pia ili waweze kufanya biashara zao mbali mbali zinazotumia umeme. Kumekuwepo na kususua kwa mradi huu wa umeme wa gridi na ujenzi wake unakwenda taratibu kwa sababu ya ufinyu wa pesa zainazotolewa Serikalini kwenda *TANESCO*:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza bajeti ya *TANESCO* ili waweze kujenga miundombinu ya umeme kwa Mkoani Katavi? (*Makof*)

Swali la pili; umeme uliopo sasa hivi Mkoa wa Katavi hautoshelezi kwa sababu kumeuwa na usambazaji wa umeme wa *REA*, hivyo watumiaji wa umeme ni wengi mkoani Katavi. Swali langu na ombi langu kwa Serikali:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutupunguzia muda wa ukamilishaji wa ujenzi wa umeme wa gridi badala ya kuwa 2023 uwe 2022? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati tafadhalii.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua kuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ambayo imeianzisha na ile ambayo imeikuta ikiwa inaendelea, nasi tuna uhakika kwamba fedha iliyopo *TANESCO* itaendelea kutosha na pale ambapo watapungukiwa Serikali itaongeza. Katika bajeti ambayo Bunge lako limepitisha jusi, takribani shilingi billioni 35 zilitengwa kwa ajili ya kuendelea na hii kazi ya ujenzi wa hiyo njia ya msongo wa kilovolti 132 kutoka Tabora kwenda Mpanda.

Mheshimiwa Spika, tunaamini fedha hizo zitatosha na kwa kadri itakavyohitajika kutoka kwa wataalamu basi Serikali itaongeza pesa hizo kwa sababu inazo.

Mheshimiwa Spika, kwenye swalii la pili, kwa kuwa wenzetu wa Katavi hawajafikiwa na gridi; na gridi kwa mujibu wa ratiba ya *TANESCO* iliyowekwa kwa mchanganuo ule wa kitaalamu wa kwamba tuanje kupembua njia ya kuitishaa umeme tulipe fidia, tujenge majengo tuchukue na hatua nyengine; naomba Bunge lako Tukufu, liruhusu na kuielekeza

Wizara iende ikakae na kuona kama muda huu unaweza ukaminywa kwa kuzingatia matakwa ya kitaalamu na bajeti tuliyojipangia ili wenzetu wa Katavi waweze kupata gridi hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, niongeze kwamba Mkoa wa Katavi unatumia umeme karibia Megawati 1 na kilowati kama 200, tutaenda kuona namna ambavyo tunaweza tukaongeza mashine na mitambo ya kuweza kufua umeme zaidi katika eneo hilo katika kipindi hiki ambacho bado tunaendelea na utengenezaji wa miundombinu yetu ya kufikisha gridi katika Mkoa wetu wa Katavi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Tabasamu. Swalii la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nami naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Sengerema imekuwa inakatika umeme mara 30 kwa siku na tayari umeme umeshatengenezwa katika eneo letu la kupoozea umeme pale Pomvu Geita, kwa nini Sengerema msituunganishe katika laini ya Geita ili tukaacha kukatikiwa umeme kwa mfumo huu wa kukatika mara 10 kwa siku?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tabasamu, Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Mbunge kwa adha ambayo wananchi wake wamekuwa wakiipata, lakini kama nilivyosema tangu awali, Serikali imepambanua kwa muundo na msukumo mpya uliopo, haya matatio makubwa yataaenda kupunguzwa katika maeneo yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kukatika umeme kama nilivyosema, kunaweza kusababishwa na laini ya umeme kuwa ndefu au mazingira mengine kwa na vitu hatarishi kama

maeneo ambayo ni oevu na tunafahamu maeneo mengi ya kanda ya ziwa ni oevu, kwa hiyo, nguzo zetu zimekuwa zikianguka au pengine laini kuwa na watumiaji wengi na pengine ikazidiwa. Kwa hiyo, mambo yote hayo yanachukuliwa maanani na kuangalia namna gani ambavyo tutaweza kurekebisha katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Tabasamu aniruhusu baada ya hapa nikae nae niongee naye nichukue eneo lake kazi, ili nikakae na wataalamu tuweze kujua tatizo hasa linasababishwa na nini katika sababu mbalimbali. Maana inawezekana ukajenga kituo cha kupooza umeme katika eneo hilo, lakini bado umeme ukaendelea ukakatika kwa sababu tatizo halikuwa kituo cha umeme, pengine ilikuwa tatizo lingine, tukibaini tatizo lenyewe tutaweza kulifanyia kazi kwa usahihi.

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaona mna maswali mengi sana ya umeme. Tafsiri yake ni kwamba mambo haya ya kukatika kwa umeme limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nawaomba Kamati ya Nishati na Madini kwa niaba yetu, hebu kaeni na hii Wizara, mridhishwe na mipango iliyopo na hiyo Bodi iiteni wajue uzito wa kazi waliyopewa. Vinginevyo tatizo ni kubwa sana.

Na. 8

### **Kurejesha Ardhi ya Kijiji cha Nyarututu/Kabanga – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutaka mwananchi aliyevamia ardhi ya Kijiji cha Nyarututu/Kabanga kurejesha ardhi hiyo kwa Serikali ya Kijiji ili itumike kwa faida ya wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali, tafadhali. Nawaruhusu Wahehimiwa mawaziri mjibu tu kutoka kwenye maeneo yenu. Tafadhali nawaruhusu sana, ili tuendelee na utaratibu wetu

ule wa kulindana kidogo. Wwabaki watoa hoja na wanaoweka hati Mezani. Karibu Mheshimwa Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ardhi ya Kijiji cha Nyarututu yenye ukubwa wa ekari 130 ilipangwa na Serikali ya kijiji cha Nyarututu kwa matumizi ya Umma. Hata hivyo, kumekuwa na mgogoro unaoendelea ambapo Bwana Zacharia Kabutelana amefungua kesi dhidi ya vlongozi wa kijiji akidai kwamba aliwahi kupewa eneo hilo na Serikali ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Bwana Zacharia amefungua maombi Baraza la Ardhi na Nyumba katika Shauri Na. 18/2019 ambapo lipo kwenye hatua za kusikilizwa. Kutokana na eneo hilo kuwa na maslahi ya Umma, Mkurugenzi amepeleka maombi Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ili naye awe sehemu ya kesi hiyo na kuwakilishwa na Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya. Afisa Ardhi wa Halmashauri hiyo ameagizwa kufuatilia kwa karibu shauri hili ili kuhakikisha maslahi ya Serikali yanalindwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, nimekuona.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za Serikali ikiwemo afya pamoja na shule, yamekuwa yakivamiwa na watu ambao hawana nia njema:-

Serikali ina mpango gani maeneo haya yote ili yaweze kupimwa kuondoa hii adha ambayo imekuwa ikijitokeza? (*makofi*)

Swali la pili; tunayo miji midogo kama Nkwenda, Nsingiro, Mrongo na Mabira. Maeneo haya yanakua kwa kasi: Serikali ina mpango gani wa kupima haya maeneo ili baadaye wasije wakaanza kuwavunja wananchi nyumba zao? (*makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri kwa Mbunge wa Kyerwa, maswali yanayowahusu wananchi hayo.

**WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Naomba nijibu mawali mawili ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli uvamizi ni mkubwa sana katika maeneo mbalimbali, lakini nilitaka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji, Mamlaka ya Upangaji wa Ardhi ni Halmashauri za Wilaya. Maana yake ni kwamba ukipanga unapaswa kusimamia, wanaopanga *master plan*. Wanaopanga mipango flani flani ya utekeleaji wa *master plan* ndani ya sheria za nchi hii ni Halmashauri ndio wanaohitaji na ndio wanaojua kwamba ardhi yao itumike namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa Halmashauri zote, zisimamie na zilinde maeneo kama yalivyopangwa na mamlaka zao. Maeneo yote ya wazi hayapaswi kutumika kwa shughuli nyingine na nimeelekeza wenzangu kwamba maeneo yote ya Umma kama yanaangukia kwenye sekta fulani, basi sekta hiyo iyalinde, ichukue hati na iweke mipaka inayoonekana/alamu zinazoonekana, kama ni maeneo ya shule wayalinde wachukue hati, nasi tulisema hatutawadai kodi ya ardhi ya kila mwaka. Kama ni maeneo ya afya, basi yalindwe, yapimwe yachukuliwe hati na yawekewe alama zinazonnekana ili wananchi waweze kujua. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuyalinda.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli kutokana na ustaarabu na utekelezaji ulio mzuri wa sera za CCM na llani ya Chama cha Mapinduzi, leo tuna umeme kila kijiji. Umeme unaleta ustaarabu na unabadilisha maisha. Kwa hiyo, imetokea kwamba baadhi ya vijiji vingi sasa vimeanza tabia ya kimji. Sheria inaelekeza kwamba maeneo hayo, Halmashauri myawahi mapema. Maeneo ambayo mnajua yameanza kuchipukia na maisha yanakuwa ya kimji, pelekeni na mjadili kwanza muainishe maeneo hayo hata kama ni ya vijiji, mpelekeeni Waziri wa Ardhi ayatangaze kama *town planning areas* ili maeneo hayo ya vijiji yanayochipukia kuwa na maisha ya kimji, Waziri ayatangaze ili yapangwe kimji na Halmashauri zipime na watu wapewe viwanja na hati kama za mjini. Kwa namna hiyo tunaweza tukalinda, baadaye kukawa hakuna *squatter* katika mji yetu. Kwa hiyo, ni jukumu letu Mheshimiwa Mbunge Halmashauri na sisi kama Wajumbe tusimamie katika kupanga na kusimamia ardhi yetu.

**SPIKA:** Nitoe wito tu kwa Wizara ya hizo ambazo zimetolewa kwenye uwajibikaji wa moja kwa moja wa Halmashauri *including* ardhi, yatilewe maelekezo vizuri waelewe kule chini kwa sababu mahali pengine unakuta wanakwambia sisi hatuitiki huko bwana, sisi ni Katibu Mkuu moja kwa moja. Kwa hiyo, inakuwa shida kujua Halmashauri ina mamlaka gani na hawa ambao hawaii kwa inakuaje kufanya kazi kwa pamoja na zile nyingine pia; maji, ujenzi na wengine.

Katiba na Sheria, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega.

Na. 9

### **Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Busega**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwa Wilaya ya Busega kujengewa Mahakama ya Wilaya ili kuondoa

usumbufu ambao wananchi wanaupata kwa kusafiri hadi Wilaya ya Bariadi kufuata huduma hiyo?

**SPIKA:** Katiba na Sheria majibu tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama ya Busega ni moja ya miradi itakayojengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mkandarasi wa ujenzi wa Mahakama hii amepatikana ambaye ni *United Builders* na kukabidhiwa eneo la ujenzi mwezi Oktoba. Kazi za ujenzi zimeanza na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza programu ya maboresho ya majengo ya Mahakama zake na kukarabati majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali za Mahakama hapa nchini ili kusogezza huduma karibu na wananchi na kuboresha mazingira ya kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mahakama inajengwa, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali kwa hatua za haraka ilizochukua. Ninavyozungumza sasa tayari msingi wameshaanza kuchimba. Pamoja na hayo, kwa kuwa kutoka Busega kwenda Bariadi ambako sasa kesi hizi zinaendeshwa za Kiwilaya ni kilometra takriban 70 na pale Makao Makuu ya Wilaya tuna jengo la Mahakama ya Mwanzo.

Je, Serikali sasa haioni haja ya kuturuhusu kutumia jengo lile angalau kwa hiki kipindi ambapo bado tunasubiri jengo letu kukamilika, kusikiliza kesi za kiwilaya ili kuondoa huu

usumbufu wa wananchi kwenda Bariadi na kutumia ghamama kubwa ambazo wakati mwingine wanashindwa kuzimudu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Hawa Wanyantuzu wanapenda sana kesi, hawa Wasukuma. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe, Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, pale kuna Mahakama ya Mwanzo, lakini vigezo vile vya kuitumia kama Mahakama ya Wilaya ndiyo kidogo vinakinzana, kwa hiyo waendelee kuvumilia ili tutakapokamilisha jengo lenye sifa, waweze kuanza kulitumia rasmi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, nimekuona.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Changamoto ambayo inawapata wananchi wa Busega inafanana kabisa na changamoto ambayo inawapata wananchi wa Jimbo la Momba.

Je, ni lini Serikali itaona kuna haja ya kutupa upendeleo ili tuweze kupata Mahakama yenye hadhi ya wilaya ili kuwapunguzia wananchi changamoto ya mwendo mrefu kufuata huduma za Mahakama kutoka Jimbo la Momba mpaka Mji wa Tunduma? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, bado tuko kwako Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Godfrey Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Condester Sichalwe kutoka Jimbo la Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi katika Mpango Kazi wa kuendeleza ujenzi wa hizi Mahakama zetu za wilaya, 2022/2023 tunakwenda kuanza ujenzi wa Mahakama yake ya Mombasa ili kumpunguzia hiyo adha ambayo wananchi wanaikabili kwa sasa.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mambo ya Ndani ya Nchi sasa. Swali la Mheshimiwa Mbunge wa Makunduchi, Mheshimiwa Ravia Idarus Faina.

Na. 10

### **Ujenzi wa Ofisi za Nida – Wilaya ya Kusini Unguja**

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi za *NIDA* katika Wilaya ya Kusini Unguja?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, nimekuona.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Ofisi za Wilaya kwa ajili ya kuwafikishia wananchi huduma za usajili na utambuzi wa vitambulisho karibu na maeneo yao. Katika kutekeleza mpango huo, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) imefanikiwa kufungua ofisi 150 katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *NIDA* katika Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja itajengwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Faina, swali la nyongeza.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, *NIDA* walikuwa na mashine mbili za kuzalishia vitambulisho. Wakaomba kuongeza tena na mashine mbili kwa ajili ya kuzalisha vitambulisho vya Taifa. Sasa je, ni kwa nini uzalishaji na usambazaji wa vitambulisho hivyo umepungua kwa kiasi kikubwa sana na je, hawaoni wametumia fedha za wananchi vibaya sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Radhia Idarus Faina, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikuwa na mashine mbili ambazo zilikuwa zinazalisha vitambulisho vichache kwa muda mrefu, lakini tukaomba fedha kuititia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukanunua mashine nyingine mbili na mashine hizi zikawa zinazalisha vitambulisho hivi kwa haraka kama ambavyo tofauti na mara ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyokwambia shughuli za usajili, utambuzi na utoaji wa vitambulisho hivi unaendelea mpaka ilipofika tarehe 12 Oktoba, tulishakuwa na vitambulisho karibu 10,000,000 ambavyo viko tayari na muda wowote vinategemewa kwenda kusambazwa kwa wananchi. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba mashine hizi zinafanya kazi na vitambulisho vitapelekwa kwa wananchi hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia fedha vibaya, hakuna fedha iliyoingia katika akaunti ya *NIDA*, aidha kwa Serikali au kutoka kwa wafadhili ikatumiwa vibaya. Hivyo nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha zote zilizoingia kwenye akaunti ya *NIDA* zimetumika *accordingly*. Nakushukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Pamoja na majibu hayo mazuri, Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama witeni *NIDA*. (*Makofii*)

Hawafanyi kazi nzuri, ndiyo kazi yenu Waheshimiwa kupitia hizi Kamati. Witeni kieleweke. Tumeanza nao kitambo sana *NIDA*, kupitia Kamati tutajua nini kinachoendelea huko, ndiyo maana labda Mbunge anahisi kuna hela zimeliwa.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, tafadhali.

Na. 11

### **Hitaji la Soko la Tumbaku**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo sugu la soko la zao la tumbaku nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, soko la tumbaku linategemea mahitaji katika soko la dunia. Mahitaji ya tumbaku na bidhaa zake yamekuwa yakishuka katika Soko la Dunia kwa wastani wa asilimia sita hadi saba kwa mwaka. Hali hiyo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kampeni ya kidunia ya kupunguza uzalishaji na matumizi ya tumbaku pamoja na bidhaa zake, pamoja kuanza matumizi ya sigara aina mpya inayotumia kilevi cha kutengeneza maabara (*Laboratory nicotine*) iitwayo *e-cigarette*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania inaendelea kutafuta masoko ya tumbaku kwa kuwashawishi wanunuzi waliopo kuongeza kiwango cha ununuzi kwa njia ya mkataba, kutafuta wanunuzi wapya na pia kutafuta masoko mengine mapya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hizo, wanunuzi wakubwa wameongeza ununuzi wa tumbaku kutoka kilo 39,000,000 katika msimu wa mwaka 2017/2018 hadi kilo 57,000,000 msimu wa mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la asilimia 46. Serikali imehamasisha wanunuzi wapya na kwa msimu wa 2021 kampuni nane za kizawa zilingia mkataba na wakulima kununua kilo 17,000,000. Katika hatua nyingine Serikali imeendelea kutafuta masoko mapya ambapo, Serikali inaendelea kutafuta soko la China na tayari walileta aina ya tumbaku wanayotaka na majaribio yamefanyika na sampuli ya tumbaku hiyo imepelekwa kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kutafuta masoko zinaendelea katika nchi mbalimbali, Serikali inaamini kuwa baada ya muda mfupi tatizo la soko kwa wakulima wa tumbaku wa Tanzania linaenda kupungua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, nimekuona.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni pale ambapo Serikali imesema kwamba mwaka huu kulikuwa na kampuni nane za wazawa zimeingia mikataba na wakulima. Hadi ninaposimama hapa Bungeni mwaka huu kumekuwa na kuvunja rekodi ya kuwakopa wakulima maana yake wameuza tumbaku yao mwezi wa Tano, lakini hadi ninaposimama Bungeni hapa asilimia zaidi ya 50 ya wakulima hasa waliouza tumbaku yao kwenye kampuni hizo za wazawa hawajalipwa. Hawajalipwa kwa sababu kampuni hizo ndogo zimepata shida na changamoto katika kuza tumbaku hiyo kwenye soko la dunia. Walikuwa wanauza kupitia Zambia,

wamefungiwa huko. Walikuwa wanauza kupitia Malawi, wamefungiwa huko. Sasa je, Serikali haioni hasa kama Waziri, haioni umuhimu wa kukutana na hizo kampuni nane ili kuona namna ya kuwasaidia ili hatimaye nayo yawalipe wakulima haraka iwezekanavyo? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa mujibu wa sheria, zao la tumbaku linaendelezwa na kusimamiwa na Bodi ya Tumbaku. Tangu mwaka jana Bodi ya Tumbaku imemaliza muda wake, hadi sasa hivi inafanya kazi zake kinyume cha sheria. Hivi Serikali haioni kwamba inatakiwa iteue Bodi ya Tumbaku kesho? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili tafadhalii, Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuona.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ya Kilimo imeshakutana na kampuni zote nane za Kitanzania zinazonunua tumbaku na ningeomba tu-*acknowledge* kazi iliyofanywa na kampuni hizi za Kitanzania katika kununua tumbaku. Tumbaku yote iliyonunuliwa mpaka msimu unakwisha ni jumla ya bilioni 86. Fedha zilizolipwa mpaka sasa ni bilioni 82, kwa hiyo, slo sahihi kwamba zaidi ya asilimia 50 kwamba wakulima hawajalipwa. Tuna-*acknowledge* fedha ambayo haijalipwa ya wakulima mpaka sasa imebaki shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwenye eneo hili tumbaku hii iliyonunuliwa na naomba Bunge lako Tukufu lifahamu kabla ya kuleta kampuni za Kitanzania katika mfumo wa ununuzi wa tumbaku pamoja na *grade* zaidi ya 60 za tumbaku, kulikuwa kuna tumbaku inaitwa *reject* inayotupwa ambayo mkulima anaitupa shambani. Ni kampuni hizi za Kitanzania ndio zimeenda kuinunua mpaka tumbaku inayoitwa *reject* na kwa mwaka huu hakuna tumbaku iliyobaki mikononi mwa wakulima. Kunapokuwa na *success story*, tu-*acknowledge*

na hili ni jambo jema. Kwa miaka mingi sekta hii imekuwa kwenye *dominance* ya kampuni mbili tu. Tumeingiza kampuni za Kitanzania *against all efforts* za *international market* ambazo zilituzuia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo yaliyobaki na tumbaku iliyoko Malawi na Zambia, Balozi Simba aliyeo Zambia ameshafanya jitihada kwa sababu *walio-block* tumbaku yetu isinunuliwe Zambia ni hizi hizi kampuni kubwa zilizoko ndani ya nchi, zimetumia *subsidiary companies* zao kule nchi kuzuia tumbaku yetu isinunuliwe. Tatizo hili tumeli-*resolve*, tuko kwenye hatua za mwisho. Tumeongea na Benki ya CRDB na NMB watatoa fedha ili kampuni hizi zimalizie bilioni nne iliyobaki ambayo haijalipwa kwa wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kusema tutaendelea ku-*support* kampuni za Watanzania kununua *green tobacco* na kui-*export* kwa sababu tumbaku haiwezi kugeuka kuwa chapati.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kuhusu suala la Bodi. Bodi ya Tumbaku imemaliza muda wake, ni kweli. Sisi kama Wizara tumeshapeleka mapendekezo *vetting* inaendelea na tumeshaomba kwa Mheshimiwa Rais ili aweze kumteua Mwenyekiti. Iko kwenye hatua za mwisho na ni *interest* yetu sisi kama Wizara kuhakikisha Bodi ya Tumbaku inafanya kazi yake kwa mujibu wa sheria. Sasa hivi Bodi haipo, Mkurugenzi anafanya kazi chini ya Katibu Mkuu kwa mujibu wa sheria.

Kwa hiyo, Bodi ya Tumbaku inafanya kazi chini ya *DG* na anaripoti moja kwa moja kwa Katibu Mkuu. Tumeshapeleka mapendekezo na tunaendelea kufuatilia Serikalini.

**SPIKA:** Bado tupo Wizara ya Kilimo, lakini mtaona swali linalofuata la Mheshimiwa Stella Fiyao ambalo linasema, je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na bei kubwa ya mbolea nchini? Ni swali kubwa na swali zito. Kwa hiyo, tukuombe Mheshimiwa Stella hebu liachie meza. Hili ni swali la Bunge Zima. (*Makof*)

Katika mambo muhimu ambayo tunatarajia Serikali itakuja katika kipindi hiki sio kirefu kijacho, kuja kulitolea ufanuzi ni pamoja na hili, kwa sababu bei imepanda toka wastani wa 55,000 hadi 60,000 ya mwaka jana kwenda 110,000 hadi 120,000. Bei ambayo kwa vyovoyote vile wakulima wetu hawawezi kumudu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba hali hiyo ikiendelea na hali hii kwamba mwaka huu hali ya hewa wanatuambia huenda mvua zikawa za wastani sana na mbolea hakuna, tunaweza tukawa na janga kubwa la njaa mwakani. (*Makofii*)

Kwa hiyo, jambo hili ni kubwa. Tunai-*engage* Serikali iliangalie kwa undani wake na kabla ya Bunge hili la Tano halijaisha, tutapata maelezo ya kutosha kuhusu jambo hili kwa sababu ni jambo zito. Nashukuru.

*(Swali Namba 12 halikujibiwa kwa maelekezo ya Spika)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali la Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Na. 13

#### **Majengo Yaliyoachwa Kutumika Kama Chuo cha VETA**

**MHE. ALLY Y. MHATA** aliuliza:-

Je Serikali ina mpango gani wa kuyatumia majengo yaliyoachwa na Kampuni ya Ujenzi ya China yaliyopo Kijiji cha Maneme yatumike kama Chuo cha Ufundji (*VETA*)?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, nimekuona tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** aliibusi:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la

Mheshimiwa Ally Yahaya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundı Stadi katika Wilaya zote hapa nchini. Kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundı Stadi katika Wilaya 29 ambavyo viro katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majengo yaliyoachwa na mkandarasi aliyejenga barabara yapo na Wilaya imeona umuhimu wa kuyatumia, Wizara yangu itatuma wataalam kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi (*VETA*) washirikiane na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kufanya tathmini ya majengo hayo iwapo yanakidhi vigezo vya msingi vya kuanzisha mafunzo ya ufundı stadi.

Mheshimiwa Spika, wakati juhudı hizo zikiendelea, nashauri wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu kutumia Vyuo vya Ufundı Stadi vya Mtwara, Lindi na Namtumbo ambavyo viro jirani na Wilaya hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY Y. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri kuhusiana na swali hili, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Kijiji cha Maneme ambapo ndipo yalipo majengo haya kilishaandika barua kukabidhi majengo haya kwa Serikali. Mimi kama mwakilishi wao niliwasilisha barua yao ya kukabidhi hili eneo kwa Wizara. Kwa hiyo, nataka kupata *commitment* ya Serikali. Ni lini watendaji hawa wa Serikali watakuja ndani ya wilaya yangu ili kuyahakiki majengo haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa suala hili la ujenzi wa Vyuo vya *VETA* liko ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na sisi wananchi wa Jimbo la Nanyumbu tunayo

majengo tayari, je, Serikali haioni haja kwa Mwaka ujao wa Fedha majengo haya yakatumika ili wananchi wa jimbo langu wakanufaika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tayari timu yangu ya wataalam kutoka Wizara itakwenda eneo hili. Mheshimiwa Mbunge anataka kujua lini, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwa vile tuko hapa Bungeni na Makao Makuu ya *VETA* yako hapa Dodoma, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kipindi hiki tuweze kuonana, twende wote kwa Mkurugenzi wa *VETA* pale ofisini, twende tukaipange vizuri ili tujue wataalam wetu wale lini watakwenda kwenye eneo hili la kuweza kufanya tathmini ya pamoja na kujua kitu gani cha kufanya kule Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili, kwamba majengo yapo, kuna baadhi ya miundombinu itahitaji kuongezwa; naomba hili tulichukue tuweze kuangalia katika bajeti ijayo iwapo kama itaturuhusu kuweza kuingiza bajeti ya kuongeza miundombinu katika eneo hili. Wakati tathmini hii ikishafanyika itatupa dira ya wapi tunakoelekea, mahitaji gani yatakayohitajika na ni *commitment* gani itahitajika ya kifedha kuweza kwenda kuongeza miundombinu kwenye eneo hili. Kwa hiyo hili tunaomba tulichukue tutaenda kulifanya kazi na baada ya tathmini yetu hiyo tutakutana na Mheshimiwa Mbunge kumwonesha kitu gani tunachoweza kukifanya kwenye eneo hili. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu mazuri kabisa. Isipokuwa jambo moja Mheshimiwa Waziri, *line of authority* inataka Mkurugenzi wa VETA aje awakute wewe na Mheshimiwa ofisini kwako, siyo wewe na Mheshimiwa muondoke mwende

kwa Mkurugenzi wa VETA. Kwa hiyo ni hilo tu. Mheshimiwa Godwini nimekuona, uliza swali lako la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya wananchi wa Nanyumbu inafanana kabisa na changamoto ya wananchi wa Jimbo la Mlimba pale Kata ya Mchombe.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mchombe tayari tuna majengo pale. Huko awali kulikuwa na kituo kidogo cha VETA na vijana walikuwa wakijifunza pale, sasa kituo kile kilifungwa na majengo yale hayatumiki.

Je, Wizara haioni umuhimu inavyoenda kufanya tathminni Nanyumbu hiyo timu ya wataalamu ikafanya pia tathmini pale Mlimba Mchombe, kwa sababu majengo ya Serikali yanaendelea kuharibika tu?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Nafikiri hilo anaomba tu kwamba katika tathmini hiyo na Mlimba nako hiyo timu inaweza ikapitia tu huko. Majibu labda kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kunambi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoeleza kwenye utangulizi wako Mheshimiwa Kunambi nadhani wakati tunaunda hii timu kwa vile barabara ni hiyo hiyo moja ya kwenda Nanyumbu nadhani ni lazima tupite Morogoro, tutaona busara itakavyotutuma nadhani timu hii itapita katika eneo hilo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaenda na fedha na mipango swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rarya. Mheshimiwa Jafari!

Na. 14

### **Kuboresha Mpaka wa Kirongwe**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaboresha mpaka wa Kirongwe kwa kujenga *One Border Post* ili kuimarisha na kuongeza mapato ya Serikali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Engineer Hamad Masauni Yusuph, tafadhal!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rarya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuboresha mpaka wa Kirongwe kwa kuweka miundombinu wezeshi itakayotoa kutoa huduma kwa pamoja. Aidha, katika mwaka 2021/2022, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi million 407 kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa nyumba za makazi za watumishi Kirongwe. Vilevile, katika mwaka 2022/2023 Serikali imepanga kuboresha mipaka mbalimbali nchini ikiwemo mpaka wa Kirongwe ili taasisi za Serikali ziweze kutoa huduma kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mipaka yetu kwa kujenga nyumba za makazi kwa watumishi wa taasisi zinazofanya kazi mipakani na ofisi za kutolea huduma kwa pamoja mipakani ili kuboresha ulinzi na usalama wa nchi na pia kuongeza mapato ya Serikali.

**SPIKA:** Swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nishukuru pia na majibu mazuri ya

Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba niulize maswali mawili ya nyogeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ucheleweshaji wa umuhimu wa eneo la mpaka wa Kirongwe si tu ina umuhimu kwa Wilaya na Halmashauri ya Ranya lakini pia ina umuhimu pia kwa Serikali kwa ujumla wake kwa sababu ya *sensitivity* ya eneo lenyewe lilivyo kati ya mpaka wa Tanzania na Kenya. Lakini mpaka sasa hakuna kifaa chochote vile vifaa tofauti naweza nikasema na counter book na kalamu kwa upande wa Tanzania na Kamba peke yake. Je Serikali haioni kuna umuhimu sasa kipindi ambacho tunakwenda kwenye bajeti ya utekelezaji wa mwaka huu kuweka vifaa vya kisasa ili kuimarisha mpaka ule lakini kudhibiti mapato yanayopotea kwenye eneo lile?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa kuwa ucheleweshaji wa eneo hili linaathiri pia mapato ya halmashauri ndani ya Jimbo letu la Ranya. Je Serikali haioni kuna umuhimu, pamoja na maboresho yanayokwenda ya nyumba za watumishi, kuweka soko kubwa la kimataifa ambalo litakuwa ni sehemu ya fursa kati ya wananchi wa Wilaya yangu ya Ranya pamoja na wananchi wa upande wa pili wa Kenya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge wa Ranya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja zake zote mbili ni za msingi sana. Hoja ya kuhakikisha kwamba tunatafuta vifaa vya kutosha ili kuwezesha huduma katika mpaka wa Kirongwe pamoja na ujenzi wa soko ni hija za msingi. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge atupe muda Serikali wakati tunakamilisha, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, hatua za ujenzi wa nyumba kwa bajeti ya mwaka huu basi na hili la

vifaa tulichukue na hili la soko lenyewe Serikali imelipokea itaangalia pale hali itakaporuhusu ili liweze kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Abbas Tarimba, uliza swali la nyongeza

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa nane mwaka huu nikiwa na Kamati ya Bajeti tulipata nafasi ya kutembelea *border postya* Namanga. Lakini katika jambo ambalo lilitushangaza ni kwamba *border post* ile haikuwa na *Cargo scanner*; na katika kuuliza tukaambiya kuna *border post* nyngine vilevile hazina *cargo scanner*, jambo ambalo linahatarisha mapato ya Serikali vilevile kuchelewesha upitishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, ningombaa Serikali itueleze ni nini msimamo wa Serikali katika kuhakikisha *border post* zote kubwa zinapata *cargo scanners* ili kuweza kuondokana na matatizo yaliyopo? Ahsante, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Yusuph Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Tarimba Mbunge wa Kinondoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko katika mpango wa miaka mitano kuanzia mwaka 2020/2021 mpaka mwaka 2024/2025, ambapo mpango huu unalenga pamoja na mambo mengine kuimarisha ama kuboresha utendaji kazi wa vituo vyetu vyote tisa vya *one stop border* kote nchini; ikiwemo kuweza kuipatia vifaa, watumishi, kuwajengea uwezo watumishi, kuweza kuviimarisha kwa njia mbalimbali. Kwa hiyo mpango huu utakapokuwa umekamilika hii changamoto za *scanner* na changamoto za vitendea kazi vingine pamoja

na mifumo ya *TEHAMA* kwa ujumla wake, maabara nakadhalika na nyingine ambazo nimezitaja zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nimwombe avute subra wakati kipindi cha utekelezaji wa mkakati huu utakapokamiliika ni imani yangu kwamba tatizo la *scanner* Namanga na maeneo mengine litakuwa imepatiwa ufumbuzi.

**SPIKA:** Nashukuru kwa majibu mazuri Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Ni kweli ukifika pale *borderya* Namanga utaona aibu kwa upande wetu jinsi malori yalivyo mengi halafu upande wa pili hakuna *congestion* yoyote ile. Kwa hiyo *something has to be done* pale.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari swali la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Mbunge wa Nsimbo Mheshimiwa Anna Lupembe kwa niaba yake nimekuona Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 15

#### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kata ya Litapunga Nsimbo**

**MHE. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu katika Kata ya Litapunga?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Engineer Andrea Mathew Kundo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kufatia mabadiliko aliyoyafanya katika Wizara ya Mawasiliano na

Teknolojia ya Habari na baadaye kuwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kunituea na kuniapisha kuendelea kuwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Taknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Litapunga ina jumla ya vijiji nane ambavyo ni Kaburonge "A", Kaburonge "B", Kambuzi "A", Kambuzi "B", Kambuzi Halt, Bulembo, Lukama pamoja na Litapunga.

Mheshimiwa Spika, Kata hii imekuwa ikipokea huduma za mawasiliano kutoka kata Jirani za Katumba na Kanoge zenye huduma ya mawasiliano ya Mtandao wa Halotel na Vodacom.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) itafanya tathmini ya kiufundi ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata ya Litapunga ili kupata uelewa wa pamoja na ukubwa halisi wa changamoto ili kuelekeza ufumbuzi unaoendana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, iwapo tathmini hiyo itabainisha kuwa utatuzi wa changamoto ya upatikanaji wa huduma ya mawasiliano iliyopo unahitaji kuwa na mnara katika kata hiyo, basi Serikali itaingiza kata hii katika zabuni zitakazotangazwa katika siku za karibuni kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta umeridhika?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyoneza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kuuliza. Katika mkoa wetu wa Iringa bado kuna maeneo ambayo yanasuasua katika mawasiliano na hasa katika ya Nyazwa, pamoja na kuwa kuna mnara wa Halotel lakini bado kabisa maeneo mengisana hakuna mawasiliano. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Mkoa wote wa Iringa kata zote zinapatiwa mawasiliano ya kutosha?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Andrew Mathew Kundo

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati Mbunge wa Viti Maalum kutoka Iringa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inafikisha mawasiliano kwa wananchi wote na kuhakikisha kwamba tunaimarisha upatikanaji wa mawasiliano. Lakini naomba kupokea changamoto hii ili tuweze kutuma wataalamu wetu wakafanya tathmini na ili wajiridhishe kchangamoto iko na ukubwa gani ili tuchukue hatua stahiki. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Salma Kikwete, uliza swali lako tafadhali

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nikupongeze kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. ((Makofit))

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu, bila mawsiliano kila kitu kinakuwa siyo sawasawa. Kwa muktadha huo; Jimbo la Mchinga lina tarafa nne ndani ya tarafa mbili angalau klidogo mawasiliano ya simu yanapatikana lakini ndani ya tarafa mbili nyingine, Tarafa ya Milola na Tarafa ya Mipingo hakuna kabisa

mtandao. Kukosekana kwa mtandao unasababisha pale kuwa kama kisiwa.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatuletea mtandao katika Tarafa ya Mpingo na Milola na hasa katika vijiji vya Mipingo, Namakwia, Namkongo, Matakwa na Kiwawa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mheshimiwa Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Salma Kikwete kwa kuendelea kuwapigania wananchi wake ili wapate huduma ya mawasiliano ili waweze kufanya shughuli zao za kibashara kama ambavyo Watanzania wangetamani.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano kwa Watanzania wote. Hivyo basi changamoto kama hii inapotokea katika maeneo tofauti tofauti basi kama Serikali ni wajibu wetu kupokea changamoto hii ili tuhakikishe kwamba wataalamu wetu tuwatume katika maeneo *specific* ili wakapate ukubwa wa tatizo na namna ambavyo tutaenda kulishughulikia kulingana na eneo husika lenyewe. Ahsante.

**SPIKA:** Tukimaliza tu maswali, bado kidogo, nimekuona Mheshimiwa Nape halafu Mheshimiwa Gambo

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Mchinga amesema, ye ye kwake ni tarafa mbili, mimi nina tarafa tano. Kati ya tarafa

tano tarafa tatu hazina mawasiliano kabisa. Na utaona hapa sisi wa Lindi tunazungumzia Tarafa, siyo Kijiji, ni tarafa nzaima ambayo ina kata kadhaa na vijiji kadhaa.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuja kukomboa Mkoa wa Lindi na suala la mawasiliano kwa sababu pamekuwa na ahadi za miaka nenda, miaka rudi kulimaliza hili jambo?

Hii habari ya kusema tutakuja kutembea ndio majibu yamekuwa haya kila siku. Nataka *commitment* ya Serikali kuja kutusaidia Mkoa wa Lindi tuondokane na tatizo hili.

**SPIKA:** Dah! hii hatari hii, matarafa kwa matarafa huko, Mheshimiwa Naibu Waziri una la kusema hapo kuhusu Lindi. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Nape Nnauye Mbunge wa Mtama kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nape Nnauye kwa sababu amekuwa akitoa taarifa ya changamoto ya mawasiliano ya wananchi wake wa Jimbo la Mtama. Na kwa bahati nzuri nimekaa naye sana na tayari tumeshakubaliana mimi na yeYe tutatoka hapa kwenda mpaka Mtama kwenda kujiridisha tukiwa na wataalamu wote kiasi kwamba sasa hili tatizo pindi ambapo tutajua kwamba tatizo lipo wapi ili tuweze sasa kuingiza katika mpango wa utekelezaji wa mwaka ujao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo nilishakutaja

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa changamoto iliyopo Jimbo la Nsimbo linashabihiana kabisa na changamoto ya Jiji la Kitalii la Arusha; tunazo kata ambazo zilikuwa zamani Wilaya ya Arumeru kabla hatujawa jiji Kata kama ya Olmoti ambayo ina mitaa ya Nafco na Milongoine, Kata ya Terrat ambayo ina mitaa ya Ulepolosi,

Masikilia na Engavunet na Kata ya Olasiti ambayo ina mtaa wa Oloesho bado zina changamoto kubwa ya mawasiliano ya simu.

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu kwenye kata na mitaa hiyo ambayo nimeitaja?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrisho Gambo Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mrisho Gambo kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Arusha.

Mheshimiwa Spika, nimeshafika Arusha, na maeneo ambayo ameyataja nayatambua kweli kabisa yana changamoto hiyo. Tayari tumeshaelekeza wataalamu wetu; kwa sababu changamoto ya Arusha si ujenzi wa mnara isipokuwa ni kuongeza nguvu katika minara iliyopo ili iweze kuhudumia wakazi wa Arusha kwa sababu wamekuwa wakiongezeka kwa kasi kubwa hivyo basi minara iliyokuwepo ilikuwa imeshazidiwa nguvu. Tayari wataalamu wetu wameshaanza kufanya kazi na pindi kazi hii itakapokamillika basi changamoto hii itakuwa imeweza kutatuliwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Engineer Chiwelesa swali la mwisho kabisa kwa leo.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi pia.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Biharamulo tuna vijiji 75. Kati ya vijiji 75 vijiji 25 havina mawasiliano kabisa, kabisa, na bado tuna shida, ukiachilia mbali vitongoji. Sasa ni nini hatua ambayo Serikali imachukua kwa ajili kuweza kuboresha

mawasiliano? Ukizingatia watu hawa nao inabidi washiriki mchango wa maendeleo wa nchi hii lakini wameachwa mbali kwa sababu wako katika maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa. Nataka kusikia kauli ya Serikali kuhusu vijiji 25 vya Biharamulo.

**SPIKA:** Haya wakati Lindi ndio hivyo Biharamulo nako zaidi ya tarafa! Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ezra Mbunge wa Biharamulo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ambayo imebahatika na ambayo itanufaika katika mpango wa utekelezaji mradi wa mipakani basi na Biharamulo inaenda kupata miradi takribani sita.

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana na kuhakikisha kwamba kipindi kitakapofikia tena cha kuleta bajeti ili tuweze kuhakikisha kwamba maeneo mengi yanapata mawasiliano basi aweze kutuunga mkono kuhakikisha kwamba bajeti hii iweze kwenda kujibu mahitaji ya Watanzania. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge maswali tumalizie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambulische mgeni wa Mheshimiwa Spika, ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. Tunafarrijika Mzee Pinda unapopata nafasi ya kututembelea, tunaku-*miss* sana mjengoni. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao hamjawahi kumtembelea Mzee Pinda pale anapoishi yeye ni mkulima mzuri ni mkulima wa mfano. Sasa msiende sana maana yake sasa wageni hawa mzee ni mstaafu, sasa mkienda wengine tena mnataka kupiga na kilaji kabisa na nini, inakuwa taabu,

mナナハリブバジテヤムスタアフ。クワヒヨ、ムナボンダムエンデキドゴムメジンドー・アーダ、シムナニパタジャマニ?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ili mnamuachia na mstaafu kidogo nae, lakini kweli ana shamba zuri ni mfano mzuri wa namna ya kustaafu vizuri, Siyo mtu unastaafu una nyumba katikati ya Mji eti mstaafu! sasa hapo katikati ya Mji unafanya nini? Nenda pembezoni, tengeneza vizuri, uwe na mandhari nzuri, uwe na eneo, unaweza ukapanda hata mpapai, mchungwa, hata wajukuu wanakimbiakimbia kidogo. Sasa Mstaafu uko mahali hata eneo la watoto kucheza, wajukuu hakuna? Kwa hiyo, nawa-*encourage* katika yale mafunzo ya Jumamosi funzo moja *practical* ni kumtembelea Mzee Pinda. Karibu sana Mzee Pinda.

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunaye Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana Taifa Ndugu Kenani Kihongosi. Kwa hiyo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana amewahi kuwa Mkimbiza Mwenge Kitaifa na alikuwa Mwenyekiti wa Vijana Iringa na alikuwa *DC* Arusha, ni mchapakazi sana huyu kijana. Wale rafiki zangu wale wajiandae wasifikiri mchezo, ndiyo vijana wenye hawa. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni 12 wageni wa Spika ambaao ni Wajumbe wa Kamati ya Maadili na Kinga ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Nitawiteni mmoja-mmoja, naomba mkae tutawatambua Mbunge mmoja-mmoja:

Mwenyekiti wa Kamati anaitwa Panya Ali Abdallah ahsante sana Mheshimiwa Panya. Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis. Karibu sana, pia tunae Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Bi. Raya Issa Msellel, karibu sana Bi. Raya, hivi sasa Makatibu wa Mabunge yote mawili haya ni akinamama. Hongereni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe ni Mheshimiwa Juma Ali Khatib. Mheshimiwa Juma, karibu. Mjumbe mwingine Mheshimiwa Azza Januari Joseph. Karibu sana. Mjumbe

mwingine Profesa Omar Faki Hamad. Ahsante. Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Mjumbe. Ahsante. Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf. Ahsante. Lakini pia, tunae Mkuu wa Idara ya Shughuli za Baraza na Mshauri wa Kisheria, Ndugu Othman Ali Haji. Karibu kabisa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunae Mkuu wa Divisheni ya Kamati, Ndugu Khamis Hamad Haji. Tunao Makatibu Kamati wawili ambaao ni Ndugu Khadija Salmin Awadh na Katibu Kamati Mwanaisha Mohamed Kheir, Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe hawa wa Kamati ya Maadili wamekuja wakiwa wageni wa Kamati ya Maadili ili wajifunze namna ambavyo mambo yanavyokwenda upande huu, lakini pia Wajumbe wa kwetu nao wapate kujifunza namna wenzetu wanavyokabiliana na mambo ndani ya Baraza la Wawakilishi. Tunawakaribisheni sana, karibuni sana. Huu ni mfano mzuri sana katika kuimarisha muungano wetu na mashirikiano ya pande mbili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sioni Kamati zetu mkiomba kutembelea Baraza la Wawakilishi! Sijawazuia, ninyi wenyewe hamsemi lakini kuna mengi ya kujifunza upande wa pili. Kwa hiyo, ziara hii lazima nasi baadhi ya Kamati tu-revenge au siyo jamani? Wale watakaowahi kuleta maombi ndiyo itakuwa Kamati ya kwanza kwenda Zanzibar mara tu baada ya Bunge hili endapo Baraza linaendelea. Asante sana. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni saba wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Eliezer Feleshi ambaao ni familia yake wakiongozwa na mke wake Bi. Suzana Majija. Ngoja kwanza, kaeni kwanza, tunamhitaji Suzana, Mama watoto yuko wapi? Enhee! hongera sana shemeji. Aah, jamaa amefika hapa, sasa amewasili kwa hiyo, baada ya hapa Mama wewe endelea na shughuli zako tu ameshafika. Pamoja na watumishi wengine ambaao wametoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wale wote ambaao wamekuja kutoka katika familia tunawakaribisheni sana, karibuni sana. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Spika kutika *Zara International Travel Agency*wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa *Zara Tours*, Zainab Ansell. *Zara Tours*, karibuni sana. Ndugu Zainab ni mchapakazi sana, katika sekta ya utalii amekuwa akienda dunia nzima na kulisemea vizuri jina la Tanzania, kuweka mabanda katika mabanda ya maonesho, kuwapokea wageni kuwapeleka katika mbuga zetu. Ni mmoja wa wanamama ambaye amejitahidi sana katika kukuza eneo la utalii na tunaomba uendelee zaidi na zaidi, karibu sana *Zara*. (*Makof*)

Tunao Wageni sita wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo, kutika taasisi mbalimbali za Serikali zilizo chini ya Wizara hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege Msajis. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambaao ni familia yake wakiongozwa, sasa tunamuitaje huyu mama kwanza, Bi Neema Mgheni, eeh! kutoka Ushetu. Bi Neema amefika, umemuona alipokaa, yuko wapi? Yuko wapi Mheshimiwa? Eeh, umemuona eeh? Ahsante sana. Sasa na wewe baada ya hapa kwaheri Ushetu. Ukaangalie nyumba. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka kule Kahama, naomba Mwenyekiti na Viongozi wa CCM msimame. Ahsanteni sana. Pia, tuna Mwenyekiti wa Halmashauri na wengine kutoka Halmashauri karibuni sana. Karibuni sana na wengine wote mliotoka Ushetu na Kahama kwa ujumla karibuni sana. Tunashukuru kwa kumsindikiza Ndugu yetu. Najua mngekuja wengi sana kama siyo zuio hili la kwamba mje wachache. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. Msaidieni Mheshimiwa ili Ushetu na Kahama iweze kwenda mbele zaidi na zaidi. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mohamed Said Issa ambaao ni familia yake

kutoka Konde, Zanzibar, wakiongozwa na mke wake. Tuanze na Mama Said Issa, Wardat Juma, yuko wapi Mama? Eeh! anatoka Konde, Mama ujumbe ni ule ule. Sasa Mheshimiwa amefika kwa hiyo, wewe rudi Pemba tu yuko salama kabisa Mheshimiwa. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo kutoka Kampuni ya *Zara International* ya Mheshimiwa Zainab, ambalo anawafahamisheni Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge wanaopenda kupanda Mlima Kilimanjaro ikiwa ni lengo la kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania tarehe 09 Disemba, ambao wangependa tarehe 09 Disemba kupanda Mlima Kilimanjaro kama ilivyokuwa mwaka ule wa uhuru ilipokuwa tarehe 09 Disemba. Zoezi la upandaji wa Mlima Kilimanjaro litakuwa la siku sita kuanzia tarehe 05 taratibu, tarehe 10 kuteremka kurudi, ile tarehe 9 usiku mnakuwa pale kwenye *peak*. Kwa maelezo zaidi mnaombwa kutembelea banda ambalo wanalo hapa kwenye viwanja vyetu vya Bunge pembedni tu ya Ukumbi wa Msekwa. Ni fursa ya aina yake ni fursa ya kipekee na ni heshima kubwa endapo baadhi yetu Wabunge mtatuwakilisha katika watakaopanda Mlima Kilimanjaro kwa mkesha ule wa tarehe 9 Disemba.

Tunawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge wote, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu, ingawaje wengine watakuwa kwenye *event* ya tukio la kitaifa, lakini baadhi yetu basi wapande Mlima Kilimanjaro itakuwa ni jambo zuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie kwa masikitiko makubwa kwamba, tunaye Ndugu yetu ambaye alikuwa anasimamia masuala ya *Canteen* hapa kutoka kampuni ile ambayo inatoa huduma pale *Canteen*, anaitwa Ndugu Haruna, alifariki ghafla jana na mwili wake utasafirishwa kwenda Kigamboni kwa mazishi baadae leo, Ndugu Haruna tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amina.

Katibu. Kutengua Kanuni eeh.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**SPIKA:** Ngoja tutengue Kanuni halafu nitakupa nafasi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kwa ridhaa ya Kiti chako nitoe maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 174(1) na Kanuni ya 34(1), (2) na (3) na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mkutano wa Tano wa Bunge umeanza leo tarehe 02 Novemba, 2021 na umepangwa kumalizika tarehe 12 Novemba, 2021;

Na kwa kuwa, bado nchi yetu inaendelea na mapambano ya kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa *UVICO* 19 ambapo hatua mbalimbali za kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa huu hatari zinaendelea kuchukuliwa na kusimamiwa ipasavyo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na kwa kuwa, katika kutekeleza azma hiyo Bunge katika Mkutano wake wa Nne liliamua kupunguza muda wa vikao kwa kuanza vikao vya Bunge Saa 08:00 Mchana hadi saa 01:00 Usiku na pia, kupunguza Kipindi cha Maswali kutoka dakika 90 hadi dakika 60.

Na kwa kuwa, Kamati ya Uongozi katika Kikao chake cha Tarehe 01 Novemba, 2021 ilikubali Bunge hili liendelee na utaratibu huo hivyo kuwa na ulazima wa kutengua Kanuni ya 34(1) na (2) inayohusu muda wa Vikao vya Bunge na Kanuni ya 50(1) inayohusu muda wa kipindi cha maswali ili kuwezesha Bunge kukaa kwa muda mfupi na wakati huo huo

kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu.

Kwa hiyo basi, ili kuleta utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Tano wa Bunge, Bunge linaazimia kwamba, Kanuni ya 34(1) na (2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza Bunge kuanza Saa Tatu Kamili Asubuhi hadi Saa Saba Kamili Mchana na kurejea Saa Kumi na Moja Kamili Jioni na kuendelea hadi Saa Moja Kamili Usiku itenguliwe na badala yake Bunge lianzesa nane kamili mchana hadi saa moja kamili usiku. Aidha, Kanuni ya 50(1) ambayo inaelekeza kwamba, kipindi cha maswali kwa mikutano isiyokuwa ya bajeti ni dakika 90, itenguliwe na sasa kipindi cha maswali kiwe dakika 60.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kama ilivyo wajibu ili kuitendea haki hiyo hoja naomba niwahoji:

Wanaoafikiana na kukubali hoja hii waseme Ndiyo.

**WABUNGE:** Ndiyo

**SPIKA:** Wale wasioafiki waseme siyo

**WABUNGE:** Siyo.

**SPIKA:** Nadhani walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo, kuanzia kesho tutaendelea na utaratibu huo. Mheshimiwa Ester nilikuona.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba Muongozo wako kwa Kanuni Namba 76.

Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka na ni wewe mwenyewe ulikuwa umekaa kwenye Kiti chako wakati tunapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Wakati tunapitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge aliji-*commit* kwamba kabla ya mwaka huu kuisha ataleta Muswada wa Sheria ya Mfuko Wa Hifadhi ya Jamii kufanya marekebisho kwa ajili ya *issue* ya kikokotoo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unajua jambo hili ni la muda mrefu sana na *commitment* ya Serikali ilivyotolewa rasmi kwenye Bunge hili wafanyakazi walikuwa wanashubiri kwa hamu kubwa. Tulisema lazima Serikali ilete tufanye marekebisho ili kukubaliana na ile kauli ya Hayati Rais John Pombe Magufuli, tukasema tukiacha ile kauli peke yake siyo wote ambao wanaweza wakaifuata kwa sababu, hakuna sheria inayo-guard huo mwongozo wa Rais ambao aliutoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa hili ni Bunge. Serikali inapoji-*commit* Wabunge ni wawakilishi wa wananchi wakiwemo wafanyakazi wa Taifa hili. Sasa naomba Mwongozo wako ni lini na nimeangalia ratiba ya Bunge, hakuna kabisa tunaona wameleta marekebisho ya Muswada wa zimamoto ambao nakumbuka ultungwa kipindi hichohicho ambacho tulitunga ile sheria. Sasa je, ile *commitment* ilikuwa ya kupitisha bajeti ya Waziri Mkuu au Serikali illidanganya Bunge? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako au Serikali ilete taarifa rasmi kwa nini hawaajaleta na lini wataleta ili maslahi ya Watanzania na wafanyakazi wa Taifa hili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, nimesikia maoni na mwongozo wa Mheshimiwa Ester Bulaya naomba kusema yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Serikali yaliyotolewa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, suala hili liliipelekwa kwa Serikali na wadau wa sekta hiyo ya hifadhi ya jamii ambao ni Serikali, Wafanyakazi na Waajiri. Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kupitia Serikali alitoa kipindi cha mpito ambacho kinaisha mwaka 2022 kwenda 2023 muda ambao bado uko mbele yetu kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ilikuwa na maelekezo ya kadhaa kwanza ikiwa ni kuendelea na utaratibu ambao ulikuwa unaendelea katika kusimamia sekta ya hifadhi ya jamii kama ilivyo. Eneo jingine ilikuwa ni lazima kuhakikisha kabla ya kufanya ama kutengeneza mfumo mpya wa hifadhi ya jamii ni lazima kufanya tathimini ya kutosha wa hali ya sekta, mazingira yalivyo, kuja na mfumo ambao utakuwa endelevu kwa ustawi wa wafanyakazi, lakini vilevile kwa ustawi wa sekta yenye na kuhakikisha sekta inaendelea kudumu. Tatu ilikuwa ni eneo la kufanya mapitio ya sheria kama itaonekana kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali tulisema kwamba tunakusudia kuleta Muswada huo, lakini kwa heshima ya Bunge lako na maelekezo ambayo tumekuwa tukiyapata katika Bunge hili kwamba, sheria yoyote inayoletwa Bungeni ni lazima ifanyiwe kazi kwa viwango vya kutosha, iwe shirikishi na inapoletwa iwe ni sheria endelevu ambayo itaakisi muktadha na ustawi wa sekta inayohusiana na sheria hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa utathmini wa mifuko umekwishafanyika baada ya utathimini wa mifuko kuwa umekwishafanyika kazi ambayo inatakiwa ifanyiwe kabla ya

sheria hiyo kukamilika ni wadau wote, Vyama vya Wafanyakazi, Serikali na Vyama vya Waajiri kuipitia ripoti hiyo na kui-own kwa pamoja. Baada ya hapo sasa tukubaliane marekebisho ya sheria yanayotakiwa kufanyika yawe ni marekebisho gani ambayo yanakwenda kujibu hoja ambazo ziko mezani katika sekta ya hifadhi ya jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa busara za Serikali yetu hata kama tulikuwa tumeahidi, taarifa tutakayoileta ndani ya Bunge lako Tukufu ni kuendelea kuwaomba Wabunge watusubiri tufike muafaka na wafanyakazi na sekta husika ili jambo hili litakapokuja kuletwala Bungeni liwe ni jambo ambalo limekamilika kwa mawanda yake yote na mtizamo wake wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu Serikali iko makini sana katika kufanikisha jambo hili kwanza tukizingatia kwamba muda wa kipindi cha mpito bado tunao, lakini kubwa la pili ni lazima tuwe na maridhiano ya kutosha katika Serikali na vyama vya wafanyakazi kwa niaba ya wafanyakazi ili jambo hili liweze kwisha katika utaratibu unaotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli ni mazuri na muuliza mwongozo naye ameuliza jambo ambalo ni muhimu. Tukumbushane jambo moja tu kwamba, kwa mtu ambaye ameifanya kazi Serikali kwa miaka mingi kwa uaminifu na uadilifu, anapofikia mahali pa kustaafu halafu haelewielewi hatima yake siyo jambo jepesi, unaweza ukalichukulia ni *litekwa* sababu, halikuhusu, yaani hatima kwa sababu sasa unaondoka kwenye mazoea uliyokuanayo unaingia kwenye kustaafu.

Waheshimiwa Wabunge, watu wengi wanaogopa sana neno kustaafu na kustaafu ni usiku wa giza. Kwa hiyo, mtu unahitaji kujua kidogo unaenda kwenye maisha ya aina gani, ndiyo hiki tunachokiongelea kwa hiyo tuwaombe tu wenzetu kulipa kipaumbele kwa sababu wadau wote hao

wapo hakuna ambaye yuko nje ya nchi, kila mtu yupo. Wakutane tu kwa haraka wamalize mambo, tena hawa wa vyama vyaya wafanyakazi ndiyo wadau wenyewe wa jambo lenyewe, wamalize tu haraka waache habari ya vikao vyaya kutaka posho viwe vingi. Wafike mahali walimalize ili Bunge nasi tutende haki ili uhakika wa wastaa fu wetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wako watu unakutana nao anakuambia bwana mimi nataka 55 niache bwana kabla ya haya mambo yenu hamjabadili huko mimi hapa nataka niache. Yaani watu wanachanganyikiwa katika wafanyeje, aah! hii si ndiyo hiyo sheria yenu inayokuja hiyo ikatuletea sijui mambo gani. Watu wanachakarika wanakuwa wanakosa *direction*. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri na kwa kupitia kwako Serikali, hebu malizeni huo michakato haraka, kama unawasumbua tuleteeni Bunge sisi tutatunga. Ahsante sana. (*Makofii*)

Pia, kuna Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. Waziri wa Afya leo ameingia mitini *tactically*. Unajua huwa kuna jambo unalitenda kwa kutenda au kwa kutokutenda, sasa hili la Bima ya Afya tulishindwa miaka mitano iliyopita, tulikumbusha kila Bunge la miaka mitano, Mabunge yote 19 au 20 sasa tunahesabu la tano hili tunazidi kwenda na Mabunge ya kutunga sheria unajua ni machache sana, maana hili la mipango, linalofuata la bajeti. Kwa hiyo, Mabunge ya kutunga sheria ni machache sana tusipoyatumia Mabunge yale kutunga sheria zile ambazo ni muhimu ikawa kila siku tunakuja na *miscellaneous*, haimaanishi *miscellaneous* sio muhimu, lakini zile ambazo ni muhimu ambazo zinadaiwa na nchi kwamba, tunataka sheria hii, tena ile ambayo inadaiwa ndiyo inacheleweshwa halafu inaletwa inakuwa haipendezi. Kwa hiyo, tunaidai Sheria ya Bima ya Afya. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, hiyo maana yake ni kwamba, *earliest* hiyo ya bima ya afya, *earliest* ni Novemba mwakani, ndiyo kwa ratiba ya Bunge, si muiangalie ratiba ilivyo la sivyo inakwenda 2023 kwa ratiba yetu ilivyo. Sasa huko Serikalini huwa kuna nini kisichoisha ambacho ni michakato, michakato, michakato, kwani mnajadili nini? Si kuna

vipaumbele? Bima ya afya safari hii ndio kipaumbele namba moja cha Watanzania, agenda nyingine ni *by the way*, lakini bima ya afya ni kipaumbele namba moja. Wakati Bunge la 11 linaisha linakuja hili tulisema kabisa katika kazi mojawapo iliyoshindikana kwenye Bunge lile ilikuwa ni kutunga sheria ya Bima ya Afya kwa wote kwa hiyo, matarajio ni kwamba, Bunge hili ni lazima kabisa tutunge Sheria ya Bima ya Afya kwa wote. (*Makofi*)

Ninyi kama Wabunge mnakutana na wananchi wenye matatizo ya kiafya mengi sana wanawaomba fedha, wanawaomba hiki, lazima tufike mahali tulitazame hilo jambo, nalo tunawakumbusha tu wenzetu kwamba suala la bima ya afya mjaribu kulipa nafasi na hasa Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge wanawake ndiyo maana yangu, yaani hilo kwenu ninyi niseme zaidi hata ya sisi. Si suala la Spika sasa kulisemea, lakini kama kuna kitu mtaki-deliver kwa wamama wa Tanzania ni kuwahakikishia bima ya afya, tusaidiane katika kuvuta jambo hili. (*Makofi*)

Kamati ile ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti Mheshimiwa Nyongo, eeh, bima ya afya mzee, la sivo Kamati yako itakuwa ni *failure* kama ile iliyopita. Lazima muwaite kila wakati bima ya afya mkinyamaza kidogo tu wanaacha kwa hiyo, lazima twende pamoja mpaka hili jambo tulifikishe mahali ambapo litakuwa limekaa sawasawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii niwashukuruni sana tumekwenda vizuri, sasa tunaenda Msekwa, eeh ndiyo! Kwenye semina yetu ile kama tulivyoambiana jana na semina yetu itaongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti upo eeh?

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Ndiyo.

**SPIKA:** Eeh, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa hatua hii sasa naomba niseme kwamba shughuli zilizopangwa kwa siku ya

leo hapa mezani zimekamilika na kwa jinsi hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Nane Kamili Mchana.

*(Saa 5.15 Asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 3 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*